**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**

# MUHTASARI WA ELIMU YA DINI YA KIISLAMU KWA SHULE ZA SEKONDARI KIDATO CHA I - IV

2012

© Islamic Education Panel,2012

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa au kutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya Islamic Education Panel.

ISBN 978-9987-9524-3-4

Imebuniwa na kutayarishwa na:
Islamic Education Panel,
S.L.P 55014,
Dar es Salaam.
TANZANIA.

Simu: +255-222 450069
Faksi:+255 222 450822
Tovuti: www.islamiceducation tz.com
E-mail:info@Islamiceducation tz.com

YALIYOMO

Ukurasa

Utangulizi ......................................................................................................iii
Malengo ya Elimu Tanzania ........................................................................... iii
Malengo ya Elimu ya Sekondari .......................................................................iv
Ujuzi wa somo la Dini ya Kiislamu kwa Shule za Sekondari .........................................iv
Malengo ya kufundisha Somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu
kwa Shule za Sekondari ...................................................................................v
Muundo na Mpangilio wa Muhtasari ...................................................................v
Kidato cha Kwanza ......................................................................................... 1
Kidato cha Pili ................................................................................................9
Kidato cha Tatu ..............................................................................................17
Kidato cha Nne ...............................................................................................27

*Bismillahir Rahmaanir Rahiim*

## 1.0 UTANGULIZI

Muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu shule za Sekondari Kidato cha I-IV wa mwaka 2010 unachukua nafasi ya muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu shule za Sekondari kidato cha I - IV wa mwaka 2007. Muhtasari wa mwaka 2007 ni matokeo ya maboresho ya muhtasari rasmi wa kwanza wa mwaka 1996. Muhtasari wa mwaka 2010 ni matokeo ya maboresho ya uandishi yenye lengo la kuufanya muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu shule za sekondari kwenda sanjari na mabadiliko ya sasa ya uandishi wa mihtasari ya masomo ya shule za sekondari nchini Tanzania. Hakuna mabadiliko katika maudhui ya muhtasari wa mwaka 2007. Mambo ya msingi yaliyoboreshwa ni pamoja na mbinu za kufundishia na kujifunzia, kuongeza safu za ujuzi, upimaji na idadi ya vipindi.

## 2.0 MALENGO YA ELIMU TANZANIA

Elimu itolewayo ni ya kurithisha maarifa stadi na mielekeo bora kutoka kwa vizazi vilivyopita hadi vizazi vya wakati huu na vijavyo. Hivyo yafuatayo ndio malengo ya elimu nchini:-

1. Kuelekeza na kukuza maendeleo, kuboresha haiba ya wananchi wa Tanzania, rasilimali zao na matumizi bora ya rasilimali hizo katika kuleta maendeleo ya mtu binafsi na ya kitaifa;
2. Kukuza tabia ya kuthamini utamaduni, mila na desturi za watu wa Tanzania;
3. Kukuza upatikanaji wa fursa za kusoma, kuandika na kuhesabu na matumizi sahihi ya maarifa na stadi za kijamii, kisayansi, kiufundi, kiteknolojia, kitaalamu na aina nyingine za maarifa na ujuzi, kwa ajili ya maendeleo na kuboreshai hali ya mtu na jamii;
4. Kukuza na kuendeleza kujiamini, kudadisi, weledi na kuheshimu utu wa mtu na haki za binadamu na kuwa tayari kufanya kazi kwa kujiendeleza na kwa maendeleo ya taifa.
5. Kuwezesha na kupanua mawanda ya kujipatia maarifa, kuboresha na kukuza stadi za kiakili, ki-vitendo, uzalishaji na nyinginezo zitakiwazo katika kukidhi mabadiliko ya ki-uchumi;
6. Kumwezesha kila raia kuelewa misingi ya katiba ya nchi pamoja na kuthamini haki za binadamu na uraia, wajibu na majukumu yanayoendana nayo;
7. Kukuza utashi wa kupenda na kuheshimu kazi za kujiajiri na kuaiiriwa na kuboresha utendaji kazi katika sekta za uzalishaji na huduma;
8. Kujenga misingi ya maadili yanayokubadika kitaifa, ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na sheria kwa njia ya kujifunza;
9. Kuwezesha kuwapo kwa matumizi sahihi, usimamizi na utunzaji wa mazingira.

## 3.0 MALENGO YA ELIMU YA SEKONDARI

Nchini Tanzania elimu ya sekondari ni elimu rasmi inayotolewa kwa vijana waliomaliza darasa la saba na kupata sifa za kuingia sekondari.

Madhumuni ya elimu ya sekondari ni:

1. Kuimairisha na kupanua kina cha mawazo, maarifa, stadi na kanuni zilizojifunzwa na kukuzwa katika ngazi ya elimu ya msingi.
2. Kuimarisha ukuaji na uthamini wa umoja, utambulisho na maadili ya kitaifa, haiba, kuheshimu haki za binadamu, amali za kitamaduni, mila, desturi na wajibu wa kiraia na utayari wa kufanya kazi za kitaaluma na za mitulinga.
3. Kukuza ujuzi wa lugha na kutumia stadi za mawasiliano katika Kiswahili na angalau lugha moja ya kigeni.
4. Kutoa fursa ya kupata maarifa, stadi, mielekeo na uelewa katika nyanja teule za mafunzo.
5. Kuandaa wanafunzi kwa ajili ya elimu ya juu, elimu ya kazi, ufundi na taaluma.
6. Kuwajengea wanafunzi uwezo wa kujifunza, kujiamini, na teknolojia, maarifa na stadi za kitaaluma na za kitaalamu.
7. Kuwaandaa wanafunzi kujiunga na dunia ya kazi.

## 4.0 UJUZI WA SOMO LA DINI YA KIISLAMU KWA SHULE ZA SEKONDARI

Baada ya kufundishwa maudhui ya muhtasari huu mwanafunzi atakuwa na ujuzi wa:

1. Kutumia nguzo sita za imani katika maisha ya kila siku.
2. Kutambua mtazamo wa Qur’an juu ya dini.
3. Kubainisha sababu kwanini Uislamu ni dini sahihi.
4. Kutekeleza nguzo za Uislamu ipasavyo.
5. Kutumia sheria na kanuni za Kiislamu katika maisha ya familia na maisha ya jamii.
6. Kuthibitisha kuwa Qur’an ni kitabu kisicho na shaka kuwa kimetoka kwa Allah (s.w).
7. Kutumia ujumbe wa Qur’an katika maisha ya kila siku.
8. Kuishi kwa kumuiga Mtume (s.a.w) katika maisha ya kila siku.
9. Kutumia mafunzo kutokana na historia ya Uislamu katika kuhuisha Uislamu katika Jamii.
10. Kuchanganua mitazamo mbalimbali ya Fiqh
11. Kutatua masuala mbalimbali ya kiislamu katika jamii.

## 5.0 MALENGO YA KUFUNDISHA SOMO LA ELIMU YA DINI YA KIISLAMU KWA SHULE ZA SEKONDARI

Baada ya kufundishwa maudhui ya muhtasari huu, mwanafunzi anatarajiwa aweze:

1. Kufahamu nguzo sita za imani katika utendaji wa kila siku.
2. Kuelewa dhana ya Dini na elimu kwa mtazamo wa Qur'an.
3. Kubaini sababu kwanini Uislamu ni Dini sahihi.
4. Kuelewa namna ya kutekeleza nguzo za Uislamu.
5. Kufahamu sheria na kanuni za Kiislamu juu ya maisha ya familia na maisha ya jamii.
6. Kuelewa historia ya kushushwa na kuhifadhiwa kwa Qur'an.
7. Kutambua hoja za kuthibitisha kuwa Qur'an ni kitabu kisicho na shaka kuwa kimetoka kwa Allah(s.w).
8. Kuchambua ujumbe wa Qur'an na kuutafsiri katika maisha ya kila siku.
9. Kuelewa umuhimu wa Sunnah na Hadithi na kufafanua mafunzo ya Hadith zilizoteuliwa kwa mafunzo maalumu.
10. Kuchanganua mafunzo kutokana na historia ya Uislamu kabla, wakati na baada ya Muhammad(s.a.w).

## 6.0 MUUNDO NA MPANGILIO WA MUHTASARI

Maudhui ya somo huwasilishwa katika mada. Mada zitakazokuwa kwenye muhtasari ni zile ambazo mlengwa akijifunza anaweza kupata maarifa, mwelekeo na stadi au vitendo vinavyokusudiwa katika ujuzi ulioainishwa hapo juu. Mada zilizo katika muhtasari huu zimetokana na fani tano zifuatazo:

(i) Tawhiid
(ii) Fiqh
(iii) Qur'an
(iv) Sunnah na Hadith
(v) Tarekh

Mada kuu na ndogo zimepangwa kwa njia ya mtiririko kwa kuzingatia umuhimu wa maudhui na uwezo wa walengwa kiakili na kimakuzi. Maudhui ya muhtasari yamefafanuliwa katika vipengele vikuu saba kama ifuatavyo:

### 6.1 Ujuzi

Huu ni uwezo ambao utaonekana baada ya mwanafunzi kujifunza maudhui ya mada husika. Ujuzi huo huwa ni sehemu ya ujuzi wa jumla wa darasa husika.

## 6.2 Mada kuu/mada ndogo

Mada kuu ni eneo pana la ujifunzaji linaloibuliwa kutoka moja ya fani zilizotajwa awali. Mada hizo zimeandikwa kwa ufupi na uwazi.

Katika uandishi wa muhtasari kuna mitindo miwili ya mpangilio wa mada:-

(a) Mada inaweza kushughulikiwa kwenye darasa moja tu.

(b) Mada inaweza kushughulikiwa kwenye darasa zaidi ya moja.

Mada ndogo ni eneo dogo la ujifunzaji linalotokana na mada kuu. Mada ndogo ndizo zinazotumiwa kuibua malengo mahsusi.

## 6.3 Malengo Mahususi

Malengo mahususi hutumia kitenzi kinachopimika na yanajikita kwenye kukidhi mahitaji ya mada ndogo. Ni muhimu malengo mahususi yazingatie ngazi za majazi ya elimu na hasa ngazi zinazofikirisha zaidi. Malengo haya huzingatiwa wakati wa kupanga idadi ya vipindi vya mada ndogo.

## 6.4 Mbinu za kufundishia na kujifunzia

Mbinu za kufundishia na kujifunzia zilizopendekezwa katika muhtasari ni zile zinazomshirikisha mwanafunzi katika kujiendeleza kwa maarifa, mabadiliko ya mwenendo na stadi anuwai. Mbinu zilizotumika ni pamoja na: ziara, bungua bongo, maswali na majibu, igizo dhima, majadiliano, kumwalika mtaalamu, matembezi ya galari na onesho mbinu.

## 6.6 Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia

Hivi ni vifaa au zana anazotumia mwalimu katika kurahisisha tendo la ujifunzaji. Zana zilizomo katika muhtasari huu ni mapendekezo tu, mwalimu anao uhuru wa kubuni na kutumia zana nyingine anazoona zinafaa kulingana na urahisi wa upatikanaji na mahitaji ya darasa.

## 6.7 Upimaji

Upimaji umeanishwa kwakutumia maswali ya kumpima mwanafunzi ili aoneshe ngazi au uwezo unaotakiwa kuonekana baada ya mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Upimaji unaakisi malengo mahususi.

### 6.8 Vipindi

Kipindi ni muda unaotumika katika kufundisha somo darasani kwa wakati mmoja. Idadi ya vipindi kwa mwaka imegawanywa na kusambazwa kwenye muhtasari mzima kwa kuzingatia uzito wa mada kuu, mada ndogo na malengo mahsusi. Somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu limetengewa vipindi 4 kwa wiki ambapo kila kipindi kina dakika 40.

M. M. Wassena
Kamishna wa Elimu
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

# KIDATO CHA KWANZA

## Ujuzi wa somo la Elimu ya Kiislamu Kidato cha Kwanza

Baaada ya kumaliza Kidato cha kwanza mwanafunzi anatarajiwa kuwa na ujuzi wa:

1. Kuchanganua mtazamo wa Uislamu juu ya dhana ya elimu na dini.
2. Kubainisha nguzo za Imani na nguzo za Uislamu.
3. Kusimamisha swala.
4. Kupambanua chimbuko la Fiqh
5. Kusoma Qur'an kwa kuzingatia hukumu za Usomaji.
6. Kutambua mwenendo na matendo ya maadili ya Kiislamu.
7. Kuchanganua lengo la maisha ya mwanadamu hapa ulimwenguni.
8. Kubainisha historia ya baadhi ya mitume waliotajwa katika Qur'an.

## Malengo ya Somo la Elimu ya Dini ya Kiislam Kidato cha Kwanza

Baada ya kumaliza Kidato cha Kwanza mwanafunzi aweze:

1. Kuelewa mtazamo wa Uislamu juu ya dhana ya elimu na dini.
2. Kufahamu nguzo za Imani na nguzo za Uislamu.
3. Kuelewa sharti na nguzo za swala.
4. Kufahamu chimbuko la Fiqh.
5. Kubainisha hukumu za usomaji Qur'an na kuosoma Qur'an kwa kuzingatia ahkami.
6. Kuelewa mwenendo na matendo unaoonesha maadili ya Kiislamu.
7. Kufahamu lengo la maisha ya mwanadamu hapa ulimwenguni.
8. Kuelewa historia ya ya Mitume walioteuliwa -(Adam, Nuhu, Ibrahim, Lut, Shuwayb, Mussa, Issa).

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **1.0 MTAZAMO WA UISLAMU JUU YA ELIMU.** | 1.1 Dhana ya Elimu katika Uislamu | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza maana ya elimu katika Uislamu.<br>(b) Kubainisha sifa za mtu aliyeelimika kwa mtazamo wa Uislamu<br>(c) Kufafanua chanzo na lengo la elimu katika Usilamu<br>(d) Kubainisha umuhimu wa elimu katika Uislamu. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya bungua bongo kueleza dhana ya elimu.<br>(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kubainisha chanzo na lengo la Elimu katika Uislamu.<br>(iii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kueleza umuhimu wa elimu katika Uislamu. | - Michoro ya mifumo mbalimbali<br>- Magazeti<br>- Matini mbalimbali vya tafsiri ya Qur'an<br>- Bango kitita | Je,mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza maana ya elimu katika Uislamu?<br>(ii) Kubainisha sifa za mtu aliyeelimika kwa mtazamowa Uislamu?<br>(iii)Kufafanua chanzo na lengo la elimu katika Usilamu?<br>(iv)Kubainisha umuhimu wa elimu katika Uislamu? | 4 |
| | 1.2 Mgawanyo wa Elimu (Elimu y a Mazingira na mwongozo) | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kubainisha mgawanyo wa elimu baina ya elimu ya mazingira na elimu ya mwongozo.<br>(b) Kuhusianisha baina ya elimu ya mazingira na elimu ya mwongozo. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kubainisha mgawanyo wa elimu baina ya elimu ya mazingira na elimu ya mwongozo kwa mujibu wa Qur'an.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kuhusianisha baina ya elimu ya mazingira na elimu ya mwongozo. | - Bango kititai<br>- Msahafu<br>- Michoroya mifumo mbalimbali ya elimu | Je,mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kubainisha mgawanyo wa elimu baina ya elimu ya mazingira na elimu ya mwongozo?<br>(ii) Kuhusianisha baina ya elimu ya mazingira na elimu ya mwongozo? | 2 |
| 2.0 IMANI YA KIISLAMU | 2.1 Dhana ya Imani katika Uislamu | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza maana ya Tawhiid na matapo yake<br>(b) Kueleza maana ya imani kwa mujibu wa Qur'an.<br>(c) Kutofautisha kati ya imani katika Uislamu na imani ya dini nyingine | Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya bungua bongo kueleza maana ya Tawhiid na matapo yake<br>(i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya bungua bongo kueleza maana ya imani kw mujibu wa Qur'an.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kutofautisha kati ya imani katika Uislamu na dini nyingine. | - Chati ya matapo ya Tawhiid<br>- Matini mbalimbali za tafsiri ya Qur'an | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza maana ya Tawhiid na matapo yake.<br>(ii) Kueleza maana ya imani kwa mujibu wa Qur'an?<br>(iii)Kutofautisha kati Kutofautisha kati ya imani katika Uislamu na imani ya dini nyingine? | 4 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2.2 Nguzo za Imani | Mwanafunzi aweze:<br>(a)Kutaja nguzo sita za Imani na nguzo ya ihsan<br>(b)Kubainisha sifa za muumini wa kweli | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kutaja nguzo sita (6) za Imani katika Uislamu.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kubainisha sifa za muumini wa kweli | -Matini mbalimbali ya tafsiri ya Qur'an zinazokubalika | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kutaja nguzo sita za Imani na nguzo ya ihsan?<br>(iii)Kubainisha sifa za muumini wa kweli? | 2 |
| 3.0 MTAZAMO WA UISLAMU JUU YA DINI | 3.1 Dhana ya Dini kwa mujibu wa Qur'an. | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza maana ya Dini kwa mujibu wa Qur'an<br>(b) Kutaja aina za Dini kwa mujibu wa Qur'an.<br>(c) Kueleza maana ya Uislamu na sifa za Muislamu. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia njia ya bungua bongo kueleza maana ya ya Dini kwa mujibu wa Qur'an<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kutaja aina za Dini kwa mujibu wa Qur'an.<br>(iii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kueleza maana ya Uislamu na sifa za Muislamu. | -Qur'an tukufu<br>-Kamusi mbalimbali | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza maana ya Dini katika Uislamu?<br>(ii) Kutaja aina za Dini kwa mujibu wa Qur'an?<br>(iii)Kueleza maana ya Uislamu na sifa za Muislamu? | 2 |
| 4.0 FIQ-H | 4.1 Chimbuko la Fiqh | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza maana ya Fiqh.<br>(b) Kufafanua chimbuko la Fiqh<br>(c) Kuelezaumuhimu wa Fiqh. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya bungua bongo kueleza maana ya Fiqh<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kufafanua chimbuko la Fiqh.<br>(iii)Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia njia ya Fikirisha - jadili katika jozi kueleza umuhimu wa Fiqh. | - Matini mbalimbali ya Fiq-h | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza maana ya Fiqh?<br>(ii) Fafanua chimbuko la Fiqh?<br>(iii) Kueleza umuhimu wa Fiqh? | 2 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 4.2 Misingi ya Fiqh | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kutaja misingi ya Fiqh<br>(b) Kueleza vyanzo vya sheria ya Kiislamu. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya bungua bongo kutaja misingi ya Fiqh.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kueleza vyanzo vya sheria ya Kiislamu | Matini mbalimbali ya Fiq-h | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza misingi ya Fiqh?<br>(ii)Kueleza vyanzo vya sheria ya Kiislamu? | 2 |
| 5.0 MTAZAMO WA UISLAMU JUU YA IBADA | 5.1 Dhana ya Ibada katika Uislamu | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza maana ya ibada katika Uislamu<br>(b) Kubainisha uhusiano wa ibada maalum na maisha ya kila siku. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya bungua bongo kueleza maana ya ibada katika uislamu.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya fikiri-jozisha-jadili kubainisha uhusiano wa ibada maalum na maisha ya kila siku. | - Matini mbalimbali za tafsiri ya Qur'an | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza maana ya ibada katikaUislamu?<br>(ii)Kubainisha uhusiano wa ibada maalum na maisha ya kila siku? | 2 |
| | 5.2 Lengo la kuumbwa Mwanadamu | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza lengo la kuumbwa kwa mwanadamu<br>(b) Kueleza lengo la kuumbwa ulimwengu na viumbe wengine. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya bungua bongo kubainisha lengo la kuumbwa mwanadamu.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kueleza lengo la kuumbwa ulimwengu na viumbe wengine. | - Qur'an tukufu<br>- Kitabu cha kiada kuhusu kuumbwa kwa mwanadamu | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kubainisha lengo la kuumbwa mwan adamu?<br>(ii)Kueleza lengo la kuumbwa ulimwengu na viumbe wengine? | 2 |
| 6.0 NGUZO ZA UISLAMU | 6.1 Dhana ya Nguzo za Uislamu | (a) Kufafanua nguzo za Uislamu<br>(b) Kueleza umuhimu wa nguzo za Uislamu. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kufafanua nguzo z Uislamu.<br>(ii) Kwa kutumia njia ya maswali na majibu wanafunzi wa eleze umuhimu wa nguzo za Uislamu. | - Matini mbalimbali vya tafsiri ya Qur'an.<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza kueleza:<br>(i) Kubainisha aya na hadith zinazoelezea nguzo za Uislamu?<br>(ii) Kufafanua nguzo za Uislamu? | 2 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 6.2 Shahada | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kutamka shahada<br>(b) Kubainisha tafsiri ya shahada mbili. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kutamka shahada.<br>(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya bungua bongo kubainisha tafsiri ya shahada mbili. | - Matini ya kitabu cha kiada.<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kutamka shahada?<br>(ii) Kubainisha tafsiri ya shahada mbili? | 2 |
| | 6.3 Kusimamisha swala. | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza maana ya kusimamisha swala.<br>(b) Kufafanua juu ya utekelezaji wa sharti, nguzo na Sunnah za swala.<br>(c) Kueleza dhana ya unyenyekevu | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kujadili juu ya tofauti ya kuswali na kusimamisha swala.<br>(ii) Wanafunzi katika makundi kutekeleza kwa matendo masharti ya swala, nguzo na Sunnah za swala.<br>(iii) Mwalimu aongoze majadiliano juu ya unyenyekevu katika swala. | -Matini ya kusimamisha swala kutoka kwenye kitabu cha kiada na vinginevyo.<br>-Vifaa vya kutilia udhu.<br>-Majamvi<br>-Udongo safi | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kutofautisha kuswali na kusimamisha swala?<br>(ii) Kutekeleza masharti, nguzo na sunnah za swala?<br>(iii) Kuswali kwa unyenyekevu? | 2 |
| | 6.4 Kusimamisha Swala nyakati za dharura. | Mwanafunzi aweze:<br>Kueleza jinsi ya kuswali nyakati za dharura zifuatazo:<br>- Mtu akiwa safarini.<br>- Mtu akiwa mgonjwa.<br>- Mtu akiwa vitani. | Mwalimu kwa njia ya maswali na majibu awaoneshe wanafunzi namna ya kutekeleza swala nyakati za dharura zilizoainishwa.<br>- Wanafunzi waswali swala za dharura. | -Meza za darasa.<br>-Kuta za darasa.<br>-Matini za kusimamisha swala. | Je, mwanafunzi ameweza kueleza namna ya kusimamisha swala akiwa:<br>(i) Safarini?<br>(ii) Mgonjwa?<br>(iii) Vitani? | 4 |
| | 6.5 Kusimamisha swala za Jamaa | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza umuhimu wa swala za jamaa.<br>(b) Kueleza namna ya kuunga swala ya jamaa. | (i) Mwalimu kuongoza mjadala juu ya umuhimu wa swala za jamaa na sifa za Imamu.<br>(ii) Mwalimu kutumia wanafunzi wachache kuonesha usimamaji katika swala ya jamaa ya watu wawili, watatu, n.k. | -Jamvi<br>-Msikiti<br>-Matiniza kusimamisha swala | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza umuhimu wa swala ya jamaa?<br>(ii) Kueleza sifa za Imamu?<br>(iii) Kuunga jamaa ya watu wawili, watatu, n.k? | 2 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 6.6 Swala ya Ijumaa | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza umuhimu wa s wala ya Ijumaa.<br>(b) Kuendesha swala ya Ijumaa. | (i) Mwalimu kuongoza zoezi la kuendesha swala ya Ijumaa darasani kwa kuzingatia sharti na nguzo.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kueleza umuhimu wa swala ya jamaa. | -Khutuba ya Ijumaa iliyoandaliwa. | Je, mwanafuzi ameweza:<br>(i) Kuonesha umuhimu wa swala ya Ijumaa?<br>(ii)Kuendesha swala ya Ijumaa. | 4 |
| | 6.7 Kusimamisha swala za Sunnah | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza umuhimu wa swala za Sunnah.<br>(b) Kuainisha swala zote za Sunnah. | (i) Mwalimu aongoze majadiliano juu ya umuhimu wa swala za Sunnah.<br>(ii) Wanafunzi katika vikundi wajadili aina ya swala za sunnah. | - Vitabu vya kiada na Rejea.<br>- Bongo kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza umuhimu wa swala za Sunnah?<br>(ii)Kuainisha swala za Sunnah? | 2 |
| 7.0 QUR'AN | 7.1 Kushuka na kuhifadhiwa Qur'an | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza maana ya wahyi.<br>(b) Kubainisha aina za wahyi.<br>(c) Kueleza historia ya kushuka Qur'an.<br>(b) Kubainisha njia au namna Qur'an ilivyo hifadhiwa. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya bungua bongo kueleza maana ya wahyi na kutaja aina za wahyi.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali kubainisha njia au namna Qur'an ilivyo hifadhiwa | - Matini ya kitabu cha kiada na ziada.<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza maana ya wahyi?<br>(ii)Kubainisha aina za wahyi?<br>(iii) Kueleza historia ya kushuka Qur'an?<br>(iv) Kueleza jinsi Qur'an ilivyohifadhiwa? | 2 |
| | 7.2 Misingi ya Qur'an | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kutaja misingi ya kuifahamu Qur'an.<br>(b) Kubainisha majina ya juzuu na sura za Qur'an. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali kutaja misingi ya kuifahamu Qur'an.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia njia ya fikirisha- jozisha- jadili kubainisha majina ya juzuu na sura za Qur'an. | - Matini mbalimbali za tafsiri ya Qur'an.<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kutaja misingi ya kuifahamu Qur'an?<br>(ii)Kubainisha majina ya juzuu na sura za Qur'an? | 2 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 7.3 Usomaji wa Qur'an. | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kusoma sura zilizoteuliwa kwa kuzingatia hukumu za tajwiid.<br>(b) Kuhifadhi sura zilizoteuliwa.<br>(c) Kufafanua mafunzo ya sura zilizoteuliwa<br>(d) Kueleza umuhimu wa kusoma Qur'an kwa kuzingatia hukumu za tajwiid<br>(e) Kutaja aina za hukumu za tajwiid na kueleza matumizi yake. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi wafanye mazoezi ya kusoma sura za:<br>- Fat ha (1)<br>- Naas(114)<br>- Falaq(113)<br>- Ikhlas(112)<br>- Lahab(111<br>(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi kusoma na kuhifadhi sura zilizo teuliwa.<br>(iii) Wanafunzi wajadili katika vikundi mafunzo yanayopatikana katika sura zilizo teuliwa.<br>(iv) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi wajadili umuhimu wa kusoma Qur'an kwa hukumu za tajwiid.<br>(v) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia fikiri-jadili katika jozi kutaja aina za hukumu za tajwiid na kueleza matumizi yake. | -Qur'an tukufu<br>- Matini mbalimbali za tafsiri ya Qur'an<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kusoma sura zilizoteuliwa?<br>(ii)Kuhifadhi sura zilizoteuliwa?<br>(iii) Kufafanua mafunzo ya sura zilizoteuliwa?<br>(iv) Kueleza umuhimu wa kusoma Qur'an kwa kuzingatia hukumu za tajwiid?<br>(v) Kutaja aina za hukumu za tajwiid na kueleza matumizi yake? | 10 |
| 8.0 SUNNAH NA HADITH | 8.1 Maana na umuhimu wa Sunnah na Hadith. | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kutofautisha Sunnah na Hadith.<br>(b) Kueleza umuhimu wa Sunnah katika Uislamu. | (i) Kwa njia ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kutofautisha Sunnah na Hadith.<br>(ii)Kwa njia ya Bungua bongo wanafunzi waoneshe umuhimu wa Sunnah katika Uislamu. | - Matini juu ya Sunnah na Hadith. | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kutoa maana ya Sunnah na Hadith?<br>(ii)Kueleza umuhimu wa kufuata Sunnah? | 2 |
| | 8.2 Mafunzo ya Hadith zilizochagu liwa. | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kusoma na kuhifadhi Hadith zilizochaguliwa.<br>(b) Kubainisha mafunzo ya Hadith zilizochaguliwa. | (i) Mwalimu kutoa zoezi la kuhifadhi matini na tafsiri ya Hadith zilizochaguliwa.<br>(ii)Wanafunzi katika vikundi kujadili juu ya ujumbe wa Hadith zilizochaguliwa. | -Kitabu cha Hadith: Riyaadh Swalihina. (tafsiri ya Kiswahili) | Je mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kuhifadhi matini na tafsiri ya Hadith zilizochaguliwa?<br>(ii) Kubaini ujumbe wa Hadith zilizochaguliwa? | 4 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 9.0 HISTORIA YA KATIKA UISLAMU | 9.1 Dhana juu ya historia | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kutofautisha baina ya mtazamo wa Uislamu juu ya historia ule wa makafiri<br>(b) Kueleza mtazamo wa Uislamu juu ya lengo la na hadhi ya mwanadamu.<br>(c) Kueleza namna mwanadamu atakavyo fikia lengo la maisha na kuchukua hadhi yake | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kueleza tofauti ya mtazamo wa Uislamu na mtazamo wa makafiri juu ya historia ya ulimwengu.<br>(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia njia ya fikirisha- jozisha- jadili kueleza mtazamo wa uislamu juu ya lengo na hadhi ya mwanadamu<br>(iii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kueleza namna mwanadamu atakavyo fikia lengo la maisha na kuchukua hadhi yake ya Ukhalifa. | - Matini ya mada mbalimbali juu ya Tarekh.<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kutofautisha baina ya mtazamo wa Uislamu na juu ya historia na ule wa makafiri?<br>(ii) Kueleza lengo na hadhi ya mwanadamu?<br>(iii) Kueleza namna mwanadamu atakavyo fikia lengo la maisha na kuchu kua hadhi yake? | 4 |
| | 9.2 Historia ya Mitume walioteuliwa:<br>- Adam(a.s).<br>- Nuhu(s.a).<br>- Ibrahim(a.s).<br>- Lut(a.s).<br>- Shuayb(a.s).<br>- Musa(a.s).<br>- Issa(a.s). | Mwanafunzi aweze<br>(a) Kutaja mitume waliotajwa katika Qur'an.<br>(b) Kueleza Historia fupi ya kila mtume aliyeteuliwa na kaumu yake.<br>(c) Kuchanganua mafunzo anuai yatokanayo na historia ya mitume walioteuliwa na kaumu zao. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kutaja mitume waliotajwa katika Qur'an.<br>(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kueleza historia fupi ya kila mtume na kaumu yake.<br>(iii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kuchanganua mafunzo anuai yatokanayo na historia ya mitume walioteuliwa na kaumu zao. | Matini ya vitabu mbalimbali vya Tarekh<br><br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kutaja mitume waliotajwa katika Qur'an?<br>(ii)Kueleza historia fupi ya kila mtume na kaumu yake?<br>(iii) Kuchanganua mafunzo anuai yatokanayo na historia ya mitume walioteuliwa na kaumu zao? | 6 |

* Makafiri ni *watu wanaopinga kuwepo kwa Mwenyezi Mungu.*

## KIDATO CHA PILI

### Ujuzi wa somo la Elimu ya Kiislamu Kidato cha Pili

Baaada ya kumaliza Kidato cha Pili mwanafunzi anatarajiwa kuwa na ujuzi wa:

1. Kupambanua njia za kumtambua Mwenyezi Mungu.
2. Kutambua haja ya dini kwa mwanadamu.
3. Kufafanua mambo ya faradhi kufanyiwa maiti muislamu.
4. Kutambua swala za Sunnah.
5. Kufafanua utekelezaji wa nguzo ya Zakat, Swaumu na Hijja.
6. Kusoma, kuhifadhi na kueleza mafunzo ya sura zilizoteuliwa.
7. Kubainisha historia ya uandishi wa Hadith na sayansi ya Hadith.
8. Kufafanua historia ya kuhifadhiwa Qur'an wakati wa Mtume(s.a.w).
9. Kufafanua mafunzo yatokanayo na historia ya Uislamu kipindi cha Mtume akiwa Makkah

### Malengo ya Somo la Elimu ya Dini ya Kiislam Kidato cha Pili

Baada ya kumaliza kidato cha Pili mwanafunzi aweze:

1. Kuelewa njia ya kumjua Mwenyezi Mungu.
2. Kufahamu haja ya dini kwa mwanadamu.
3. Kutekeleza mambo ya faradhi kufanyiwa maiti Muislamu.
4. Kubainisha swala za Sunnah.
5. Kufahamu utekelezaji wa nguzo ya Zakat, Swaumu na Hija.
6. Kusoma , kuhifadhi na kueleza mafunzo ya sura zilizoteuliwa.
7. Kuelewa historia ya uandishi wa Hadith na sayansi ya Hadith.
8. Kuelewa historia ya kuhifadhiwa Qur'an wakati wa Mtume(s.a.w).
9. Kujadili mafunzo yatokanayo na historia ya Uislamu kipindi cha Mtume akiwa Makkah.

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 KUMJUA MWENYEZI MUNGU | 1.1 Njia za kumjua Mwenyezi Mungu. | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kubainisha njia za kumtambua Mwenyezi Mungu<br>(b) Kufafanua jinsi kila njia inavyomsaidia mwanaadamu katika kumtambua Mwenyezi Mungu.<br>(c) Kueleza nafasi ya wahyi katika kumjua Mwenyezi Mungu. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya bungua bongo kueleza njia za kumtambua Mwenyezi Mungu<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya fikiri jadili katika jozi kufafanua jinsi kila njia inavyosaidia katika kumtambua Mwenyezi Mungu<br>(iii)Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya fikiri jadili katika jozi kueleza nafasi ya wahyi katika kumjua Mwenyezi Mungu kwa kutoa mifano hai. | - Kitabu cha kiada cha kidato cha II | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza njia za kumtambua Mwenyezi Mungu?<br>(ii) Kueleza nafasi ya wahyi katika kumjua Mwenyezi Mungu ? | 2 |
| 2.0 MTAZAMO WA UISLAMU JUU YA DINI | 2.1 Haja ya dini kwa mwanadamu | (a) Kutofautisha baina ya mtazamo wa Uislamu na ule wa makafiri juu ya chanzo na kazi ya dini.<br>(b) Kueleza sababu kwanini mwanadamu hawezi kuishi bila dini. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya fikiri jadili katika jozi kutofautisha baina ya mtazamo wa Uislamu na ule wa makafiri ju ya dini.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi kueleza sababu kwanini mwanadamu hawezi kuishi bila dini. | | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(a)Kutofautisha baina ya mtazamo wa Uislamu na ule wa makafiri juu ya chanzo na kazi ya dini?<br>(b)Kueleza sababu kwanini mwanadamu hawezi kuishi bila dini? | 2 |
| 3.0 MAMBO YA LAZIMA KUFANYIWA MAITI WA KIISLAMU | 3.1 Kumkosha Maiti | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza hatua za kumkosha maiti.<br>(b) Kumkosha maiti. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya bungua bongo kueleza hatua za kumkosha maiti.<br>(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia igizo dhima kuonesha namna ya kumkosha maiti | - Ndoo ya maji<br>- Kata<br>- Sabuni<br>- Gloves | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza hatua za kumkosha maiti?<br>(ii)Kumkosha maiti hatua kwa hatua? | 4 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 3.2 Kumvika Maiti sanda | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza hatua za kuandaa kumvika maiti sanda.<br>(b) Kuonesha kwa vitendo namna ya kumvika maiti sanda? | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi kueleza namna ya kumvika maiti sanda<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia igizo dhima kuonesha namna ya kumvika maiti sanda. | - Vitabu mbalimbali vya Fiqh<br>- Mkeka<br>- Sanda iliyoandaliwa. | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza hatua za kumvika maiti sanda?<br>(ii)Kuonesha kwa vitendo namna ya kumvika maiti sanda? | 2 |
| | 3.3 Kumswalia Maiti | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza nguzo za swala ya maiti.<br>(b)Kufafanua hatua kwa hatua namna ya kumswalia maiti.<br>(b) Kuonesha kwa vitendo namna ya kumswalia maiti | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya bungua bongo kueleza nguzo za swala ya maiti.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi kufafanua namna ya kumswalia maiti.<br>(iii)Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia igizo dhima kuonesha namna ya kumswalia maiti. | - Vitabu mbalimbali vya Fiq-h.<br>- Mkeka<br>- Jeneza | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza nguzo za swala ya maiti?<br>(ii) Kufafanua hatua kwa hatua namna ya kumswalia maiti?<br>(iii) Kuonesha kwa vitendo namna ya kumswalia maiti? | 2 |
| | 3.4 Kumzika maiti. | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza mambo ya muhimu katika kuandaa kaburi.<br>(b) Kuonesha kwa vitendo namna ya kumzika maiti. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya fikiri jadili katika jozi kueleza mambo ya muhimu katika kuandaa kaburi.<br>(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi kueleza namna ya kumzika maiti. | Kitabu cha kiada kidato cha II | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza mambo ya muhimu katika kuandaa kaburi?<br>(ii)Kuonesha kwa vitendo namna ya kumzika maiti? | 4 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 4.0 NGUZO ZA UISLAMU. | 4.1 Shahada | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kubainisha tafsiri na maana ya shahada mbili<br>(b) Kubainisha sifa za mtu aliyetoa shahada mbili. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia maswali na majibu kubainisha tafsiri na maana ya shahada mbili<br>(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia maswali na majibu kueleza sifa za mtu aliyetoa shahada. | Kitabu cha kiada cha kidato cha II | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kubainisha maana ya shahada mbili?<br>(ii)Kubainisha sifa za mtualiyetoa shahada.? | 2 |
| | 4.2 Kusimamisha swala za Sunnah | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza umuhimu wa kusimamisha swala za Sunnah<br>(b) Kuanisha swala za Sunnah. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya bungua bongo kueleza umuhimu wa kusimamisha swala za Sunnah<br>(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kuanisha swala za Sunnah | Kitabu cha kiada cha kidato cha II | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza umuhimu wa swala za Sunnah?<br>(ii) Kuanisha swala za Sunnah? | 2 |
| | 4.3 Zakat | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza tofauti kati ya zakat na Sadaqat.<br>(b) Kuainisha masharti ya utoaji Zakat na Sadaqat.<br>(c) Kuchambua mali zitolewazo zakat, nisab na viwango vyake.<br>(d) Kubainisha makundi ya watu wanostahiki kupewa zakat | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kutofautisha kati na ya zakat na Sadaqat.<br>(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi kuainisha masharti ya utoaji Zakat na Sadaqat.<br>(iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya kuchambua mali zitolewazo zakat, nisab na viwango vyake.<br>(iv) Wanafunzi wajadili makundi ya watu wanostahiki kupewa zakat. | - Msahafu wa tafsiri.<br>- Kitabu cha kiada cha kidato cha II | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza tofauti kati na ya zakat na Sadaqat?<br>(ii)Kuainisha masharti ya utoaji Zakat na Sadaqat?<br>(iii) Kuchambua mali zitolewazo zakat, nisab na viwango vyake?<br>(iv) Kubainisha makundi ya watu wanostahiki kupewa zakat? | 4 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 4.4 Kufunga Mwezi wa Ramadhani | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kutaja nguzo, sunnah na miiko ya funga.<br>(b)Kuanisha mambo yanayoharibu na kubatilisha funga.<br>(c) Kubaini wanaoruhusiwa kutofunga Ramadhani. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kutaja nguzo, sunnah na miiko ya funga.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kuainisha mambo yanayoharibu na kubatilisha funga.<br>(iii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano wabaini wanaoruhusiwa kutofunga Ramadhani. | - Msahafuwa tafsiri.<br>- Kitabu cha kiada cha kidato cha II<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kutaja nguzo, sunnah na miiko ya funga?<br>(ii)Kuanisha mambo yanayo batilisha funga?<br>(iii) Kubaini wanaoruhusiwa kutofunga Ramadhani? | 6 |
| | 4.5 Swaumu za Sunnah | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza umuhimu wa swaumu za sunnah.<br>(b) Kubainisha swaumu za Sunnah na kueleza utekelezaji wake. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi kujadili dhana ya swaumu ya sunnah.<br>(ii)Kwa njia ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi waeleze umuhimu wa funga za sunnah.<br>(iii)Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia bungua bongo wabainishe swaumu ya sunnah na utekelezaji wake. | -Msahafu wa tafsiri.<br>-Kitabu cha kiada cha kidato cha II | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza umuhimu wa swaumu za sunnah?<br>(ii) Kubainisha swaumu za Sunnah na kueleza namna ya utekelezaji wake? | 4 |
| | 4.6 Swaumu za Kafara | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Keleza dhana ya swaumu za kafara<br>(b) Kubainisha funga za kafara na kueleza utekelezaji wake.<br>(c) Kuainisha sababu za funga za kafara. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi kujadili dhana ya swaumu za kafara<br>(ii)Kwa njia ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi wabainishe funga za kafara.<br>(iii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi wabainishe sababu za funga za kafara | -Msahafu wa tafsiri.<br>-Kitabu cha kiada cha kidato cha II | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza dhana ya swaumu za kafara?<br>(ii) Kubainisha funga za kafara na kueleza utekelezaji wake?<br>(iii) Kuainisha sababu za funga za kafara? | 2 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 4.7 Hija | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kutofautisha kati ya Hijja na Umrah<br>(b) Kueleza aina za Hija<br>(c) Kufafanua matendo ya ibada Hija na Umrah.<br>(d) Kueleza umuhimu wa siku ya Iddil haji na sunnah ya kuchija. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wa kutumia mbinu ya fikiri-jadili katika jozi kutofautisha kati ya Hijja na Umrah<br>(ii) Wanafunzi katika vikundi wataje na kujadili aina za Hija<br>(iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza umuhimu wa siku ya Iddil haji na sunnah ya kuchija. | - Msahafu wa tafsiri.<br>- Kitabu cha kiada cha kidato cha II | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kutofautisha kati ya Hijja na Umrah?<br>(ii) Kueleza aina za Hija?<br>(iii)Kufafanua matendo ya ibada Hija na Umrah?<br>(iv) Kueleza umuhimu wa siku ya Iddil haji na sunnah ya kuchija? | 6 |
| 5.0 QURA'N | 5.1 Kushuka na kuhifadhiwa kwa Qur'an | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kufafanua hatua mbili kuu za kushuka Qur'an.<br>(b) Kueleza hekima ya Qur'an kushuka hatua kwa hatua.<br>(c) Kueleza namna Qur'an ilivyohifadhiwa | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi wajadili hatua mbili kuu za kushuka Qur'an.<br>(ii) Wanafunzi katika vikundi wajadili hekima ya Qur'an kushuka hatua kwa hatua.<br>(iii) Wanafunzi wajadili jinsi Qur'an ilivyohifadhiwa | - Matini za Qura'n<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kufafanua hatua mbili kuu za kushuka Qur'an?<br>(ii) Kueleza hekima ya Qur'an kushuka hatua kwa hatua?<br>(iii) Kueleza namna Qur'anilivyo hifadhiwa? | 2 |
| | 5.2 Kusoma na kuhifadhi sura zilizoteuliwa | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kusoma sura zilizoteuliwa<br>- Nasr (110)<br>- Kafiruun (109)<br>- Kawthar (108)<br>- Mau'un (107)<br>- Quraysh (106)<br>(b) Kuhifadhi sura zilizoteuliwa.<br>(c) Kueleza mafunzo yatokanayo na sura zilizoteuliwa. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi wafanye mazoezi ya kusoma sura za:<br>-Nasr (110)<br>-Kafiruun (109)<br>-Kawthar (108)<br>-Mau'un (107)<br>-Quraysh (106<br>(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi kusoma na kuhifadhi sura zilizo teuliwa<br>(iii) Wanafunzi wajadili katika vikundi mafunzo yanayopatikana katika sura zilizo teuliwa. | - Msahafu wa tafsiri.<br>- Kitabu cha kiada cha kidato cha II | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kusoma sura zilizoteuliwa?<br>(ii)Kuhifadhi sura zilizoteuliwa?<br>(iii) Kueleza mafunzo yatokanayo na sura zilizoteuliwa? | 8 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 6.0 SUNNAH NA HADITH | 6.1 Uandishi wa Hadith za Mtume(s.a.w) | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kuchambua vipindi vinne vya historia ya uandishi wa Hadith za Mtume(s.a.w).<br>(b) Kueleza kwa ufupi historia ya maimamu walioandika sahihi sitta. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kuchambua vipindi 4 vya historia ya uandishi wa Hadith kuanzia kipindi cha Mtume (s.a.w) hadi Tabi Tabiin<br>(ii) Wanafunzi wakiongozwa na mwalimu wajadili historia za Maimamu 6 walioandika vitabu sita vya Hadith sahihi ('sahih Sitta'). | - Matini za Hadith za Mtume(s.a.w)<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kuchambua vipindi vinne vya historia ya uandishi wa Hadith za Mtume(s.a.w)?<br>(ii)Kueleza kwa ufupi historia ya maimamu walioandika 'sahihi Sitta'? | 6 |
| | 6.2 Uchambuzi wa Hadith za Mtume(s.a.w). | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kubainisha tanzu anuai za Hadith.<br>(b) Kuchambua vigezo vya uhakiki wa Hadith. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu wabainishe tanzu zote za Hadith - kv. Nabawiy, Qudus, Sahihi, Hassan, Dhaifu, Maudhuu.<br>(ii) Katika vikundi wajadili vigezo vya uhakiki wa Hadith. | - Matini za Hadith za Mtume(s.a.w)<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kubainisha tanzu anuai za Hadith?<br>(ii)Kuchambua vigezo vya uhakiki wa Hadith? | 4 |
| | 6.3 Hadith za mafunzo maalum | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kusoma na kuhifadhi Hadith.<br>(b) Kueleza tafsiri ya Hadith zilizoteuliwa.<br>(c) Kuchambua mafunzo yatokanyo na Hadith zilizoteuliwa. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi kusoma na kuhifadhi Hadith.<br>(ii) Wanafunzi katika vikundi waeleze tafsiri ya Hadith zilizo teuliwa.<br>(iii) Wanafunzi wajadili katika vikundi mafunzo yanayopatikana katika Hadith zilizo teuliwa, kwa mafunzo maalumu. | - Matini za Hadith za Mtume(s.a.w)<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kusoma na kuhifadhi Hadith?<br>(ii)Kutoa tafsiri ya kila Hadith?<br>(iv)Kuchambua mafunzo yatokanayo na kila Hadith? | 8 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 7.0 BARA ARAB ZAMA ZA JAHILIYYAH KARNE YA 6 A.D | 7.1 Bara Arab zama za Jahiliyyah. | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kuelezea jografia ya Bara Arab.<br>(b) Kueleza hali ya utovu wa maadili na ushirikina wakati wa kuzaliwa Mtume(s.a.w).<br>(c) Kueleza hali halisi ya mji wa Makka na kabila la Quraysh. | (i) Kwakutumia Ramani mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikudi kujadili jeografia ya Bara Arab.<br>(ii)Wanafunzi wajadili hali ya utovu wa maadili na ushirikiana wakati wa kuzaliwa Mtume(s.a.w).<br>(iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi kujadili mji wa Makka na kabila la Quraysh. | - Matini za historia ya Uislamu.<br>- Kitabu cha kiada cha kidato cha II<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kuelezea jografia ya Bara Arab.<br>(ii)Kueleza hali ya utovu wa maadili na ushirikina wakati wa kuzaliwa Mtume(s.a.w)<br>(iii)Kueleza mji wa Makka na kabila la Quraysh. | 4 |
| | 7.2 Kulingania Uislamu Makkah | (a) Kueleza nasaba na malezi ya Mtume(s.a.w).<br>(b) Kueleza maandalizi ya Muhammad kabla na baada ya kupewa utume na mafunzo yatokanayo.<br>(c) Kufafanua sababu za makafiri wa Makkah za kuupinga Uislamu na mafunzo yatokanayo.<br>(d) Kufafanua mbinu za makafiri za kuupinga Uislamu Makkah na mafunzo yatokanayo.<br>(e) Kueleza jinsi Muhammad(s.a.w). alivyoandaa ummah wa waislamu Makkah na mafunzo yatokanayo.<br>(f) Kufafanua mchakato wa hijra ya mtume na maswahaba kuhamia Madinah na mafunzo yatokanayo. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi kujadili maandalizi ya Muhammad kabla na baada ya kupewa utume na mafunzo yatokanayo.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kufafanua sababu za makafiri wa Makkah za kuupinga Uislamu na mafunzo yatokanayo.<br>(iii) Wanafunzi wajadili mbinu za makafiri za kuupinga Uislamu Makkah na mafunzo yatokanayo<br>(iv) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kueleza jinsi Muhammad (s.a.w) alivyoandaa ummah wa waislamu Makkah na mafunzo yatokanayo<br>(v) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kufafanua mchakato wa hijra ya mtume na maswahaba ya Madinah na mafunzo yatokanayo. | - Matini za historia ya Uislamu.<br>- Bango kitita | (i) Kueleza nasaba na malezi ya Mtume(s.a.w).<br>(ii) Kueleza maandalizi ya Muhammad kabla na baada ya kupewa utume na mafunzo yatokanayo?<br>(iii)Kufafanua sababu za makafiri wa Makkah za kuupinga Uislamu na mafunzo yatokanayo?<br>(iv)Kufafanua mbinu za makafiri za kuupinga Uislamu Makkah na mafunzo yatokanayo?<br>(v)Kueleza jinsi Muhammad (s.a.w) alivyoandaa ummah wa waislamu Makkah na mafunzo yatokanayo?<br>(vi)Kufafanua mchakato wa hijra ya mtume na maswahaba na kuhamia Madinah na mafunzo yatokanayo? | 10 |

* Makafiri ni watu wanaopinga kuwepo kwa *Mwenyezi Mungu.*

## KIDATO CHA TATU

### Ujuzi wa somo la Elimu ya Kiislamu Kidato cha Tatu

Baaada ya kumaliza kidato cha  Tatu wanafunzi anatarajiwa kuwa na ujuzi wa:

1. Kutambua  vigezo vya kuonesha kuwa Uislamu ndio dini sahihi.
2. Kuthibitisha nguzo ya kwanza ya imani hadi nguzo ya tano.
3. Kueleza aina za shirk na kina cha uovu wa shirk.
4. Kupambanua falsafa ya nguzo za Uislamu
5. Kutambua haki na uadilifu katika Uislamu.
6. Kueleza jinsi Qur’an ilivyohifadhiwa wakati wa Uthman(r.a).
7. Kuthibitisha kuwa Qur’an ni kitabu cha Mwenyezi Mungu.
8. Kutumia mafunzo ya sura zilizoteuliwa.
9. Kutumia mafunzo ya Hadith zilizoteuliwa kwa mafunzo maalumu.
10. Kutambua uanzishwaji na uendeshaji wa Dola ya Kiislamu wakati wa Mtume(s.a.w)

### Malengo ya Somo la Elimu ya Dini ya Kiislam Kidato cha Tatu

Baada ya kumaliza kidato cha tatu mwanafunzi aweze:

1. Kubainisha vigezo vya kuonesha kuwa Uislamu ndio dini sahihi.
2. Kuelewa nguzo ya kwanza ya imani hadi nguzo ya tano.
3. Kubainisha  aina za shirk na kina cha uovu wa shirk.
4. Kueleza falsafa ya nguzo za Uislamu.
5. Kubainisha haki na uadilifu na haki zitolewazo na Uislamu kwa makundi mbalimbali ya watu katika jamii.
6. Kubainisha jinsi Qur’an ilivyonakiliwa upya wakati wa Uthman(r.a).
7. Kufahamu kuwa Qur’an ni kitabu cha Mwenyezi Mungu.
8. Kufafanua mafunzo ya sura zilizoteuliwa kwa mafunzo maalum.
9. Kufahamu na mafunzo ya Hadith zilizoteuliwa kwa mafunzo maalum.
10. Kuelewa uanzishwaji na uendeshaji wa Dola ya Kiislamu wakati wa Mtume(s.a.w).

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 DINI SAHIHI ANAYOSTA HIKI MWANAAD AMU | 1.1 Vigezo vya Dini sahihi | Mwanafunzi aweze:<br>(a)Kuanisha vigezo vya Dini sahihi.<br>(b)Kueleza sababu kwanini mwanadamu hawezi kuunda dini sahihi.<br>(c)Kueleza jinsi Uislamu unavyo kidhi vigezo vya dini sahihi | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia njia ya fikiri jadili katika jozi kuainisha vigezo vya dini sahihi.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kueleza sababu kwanini mwanadamu hawezi kuunda dini sahihi.<br>(iii)Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia njia ya piramidi kueleza jinsi uislamu unavyokidhi vigezo vya dini sahihi. | - Bango kitita<br>- Kitabu cha kiada cha kidato chaa III | Je,mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kuanisha vigezo vya Dini sahihi?<br>(ii)Kutoa sababu kwanin mwanadamu hawezi kuunda dini sahihi?<br>(iii) Kueleza ni kwa vipi Uislamuunakidhi vigezo vya dini sahihi? | 4 |
| | 1.2 Jihad katika kusimamisha Uislamu | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza maana ya kusimamisha Uislamu.<br>(b) Kueleza umuhimu wa jihad katika kusima misha Uislamu. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya bungua bongo kueleza maana ya kusimamisha Uislamu katika jamii.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kueleza umuhimu wa jihad. | - Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza maana ya kusimamisha Uislamu?<br>(ii)Kueleza umuhimu wa jihad katika kusimamisha Uislamu | 2 |
| 2.0 NGUZO ZA IMANI | 2.1 Kumuamini Mwenyezi Mungu | Mwanafunzi aweze:<br>(a)Kueleza madai ya makafiri dhidi ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu na udhaifu wa madai hayo.<br>(b)Kuonesha kuwa kumuamini Allah(s.a.w) si swala la kibubusa(kufuata mkumbo)<br>(c)Kufafanua dalili za kuwepo kwa Mwenyezi Mungu.<br>(d)Kueleza athari ya kumuamini Mwenyezi Mungu katika maisha ya kila siku. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia njia ya fikiri jadili katika jozi kueleza madai ya makafiri dhidi ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu na udhaifu wa madai hayo.<br>(ii)Mwalimu awarejeshe wanafunzi katika aya za Qur'an zinazo onesha kuwa kuamini Allah(s.w) ni swala la kiakili.<br>(iii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kufafanua dalili za kuwepo kwa Mwenyezi Mungu.<br>(iv)Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kueleza athari ya kumuamini Mwenyezi Mungu katika maisha ya kila siku. | Matini juu ya kumuamini mwenyezi Mungu.<br><br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza madai ya makafiri dhidi ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu na udhaifu wa madai hayo?<br>(ii)Kuonesha kuwa kuamini Allah(s.w) ni swala la kiakili?<br>(iii)Kufafanua dalili za kuwepo kwa Mwenyezi Mungu?<br>(iv)Kueleza athari ya kumuamini Mwenyezi Mungu katika maisha ya kila siku? | 4 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2.2 Shirk | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza maana ya shirk.<br>(b) Kufafanua aina za shirk.<br>(c) Kubainisha kina cha uovu wa shirk.<br>(d) Kueleza maana ya kumuamini Mwenyezi Mungu katika maisha ya kila siku. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya bungua bongo kueleza maana ya shirk.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kufafanua aina za shirk.<br>(iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kueleza maana ya kumuamini mwenyezimungu katika maisha ya kila siku. | - Picha ya watu wakisujudia miti, milima, jua.<br>- Hirizi. | Je,mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza maana ya shirk?<br>(ii) Kufafanua aina za shirk?<br>(iii) Kubainisha kina cha uovu wa shirk?<br>(iv) Kueleza maana ya kumuamini Mwenyezi Mungu katika maisha ya kila siku? | 2 |
| | 2.3 Kuamini malaika wa Mwenyezi Mungu | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza umuhimu wa kuamini malaika<br>(b) Kufafanua sifa na kazi za malaika<br>(c) Kueleza maana ya kuamini malaika katika maisha ya kila siku. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kueleza umuhimu wa kuamini malaika.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya bungua bongo kufafanua sifa na kazi za malaika.<br>(iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kueleza athari za kuamini malaika katika maisha ya kila siku. | - Matini juu ya kuamini malaika.<br>- Kielelezo kinachoonesha sifa za malaika.<br>- Kielelezo kinachoonesha kazi za malaika. | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza umuhimu wa kuamini malaika?<br>(ii)Kufafanua sifa na kazi za malaika?<br>(iii)Kueleza athari za kuamini malaika katika maisha ya kila siku? | 4 |
| | 2.4 Kuamini vitabu vya Mwenyezi Mungu | (a) Kueleza umuhimu wa kuamini vitabu vya Mwenyezi Mungu<br>(b) Kubainisha vitabu vya Mwenyezi Mungu vilivyotajwa katika Qur'an.<br>(c) Kueleza tofauti baina ya Qur'an na Vitabu vingine vya Mwenyezi Mungu.<br>(d) Kueleza maana halisi ya kuamini vitabu vya Mwenyezi Mungu katika maisha ya kila siku. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano Kueleza umuhimu wa kuamini vitabu vya Mwenyezi Mungu.<br>(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kutaja vitabu vya Mwenyezi Mungu.<br>(iii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kueleza tofauti baina ya Qur'an na Vitabu vingine vya Mwenyezi Mungu.<br>(iv)Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kueleza maana halisi ya kuamini vitabu vya Mwenyezi Mungu katika maisha ya kila siku. | - Msahafu wa tafsiri.<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza umuhimu wa kuamini vitabu vya Mwenyezi Mungu?<br>(ii) Kubainisha vitabu vya Mwenyezi Mungu vilivyotajwa katika Qur'an?<br>(iii) Kueleza tofauti baina ya Qur'an na Vitabu vingine vya Mwenyezi Mungu?<br>(iv) Kueleza maana halisi ya kuamini vitabu vya Mwenyezi Mungu katika maisha ya kila siku? | 4 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3.0 MTAZAMO WA UISLAMU JUU YA IBADA | 3.1 Dhana ya Ibada | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza dhana ya Ibada kwa mtazamo wa Uislamu.<br>(b) Kubainisha lengo la jumla la Ibada maalumu kama swala, zakat, swaumu n.k. | (i) Kwa kutumia mbinu ya bungua bogo mwalimu awaongoze wanafunzi waeleze dhana ya Ibada kwa mtazamo wa Uislamu.<br>(ii)Kwa njia ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi wabainishe lengo la jumla la Ibada maalumu. | - Kitabu cha kiada cha kidato cha III | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza dhana ya Ibada kwa mtazamo wa Uislamu?<br>(ii)Kubainisha lengo la jumla la Ibada maalum kama vile swala, zakat, swaum? | 2 |
| 4.0 NGUZO ZA UISLAMU | 4.1 Kusimamisha swala | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza umuhimu wa kusimamisha swala<br>(b) Kubainisha lengo la swala na namna linavyofikiwa.<br>(c) Kueleza faida za kusimamisha swala.<br>(d) Kubainisha sababu kwanini baadhi ya wanaoswali hawafikii lengo la swala. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kueleza umuhimu wa kusimamisha swala.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kubainisha lengo la swala na nmna linavyofikiwa.<br>(iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kueleza faida za kusimamisha swala.<br>(iv)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kubainisha sababu kwanini baadhi ya wanaoswali hawafikii lengo la swala. | Matini juu ya kusimamisha swala | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza umuhimu wa kusimamisha swala?<br>(ii) Kubainisha lengo la swala na namna linavyofikiwa?<br>(iii)Kubainisha lengo la swala na namna linavyofikiwa?<br>(iv)Kueleza faida za kusimamisha swala?<br>(v) Kubainisha sababu kwanini baadhi ya wanaoswali hawafikii lengo la swala? | 4 |
| | 4.2 Zakat | (a) Kueleza maana na umuhimu wa zakat.<br>(b) Kubainisha lengo la zakat na namna linavyofikiwa.<br>(c) Kubainisha sababu kwanini lengo la zakat halifikiwi katika jamii yetu. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kueleza maana na umuhimu wa zakat<br>(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kubainisha lengo la zakat na nmna linavyofikiwa.<br>(iii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kubainisha sababu kwanini lengo la Zakat halifikiwi katika jamii yetu. | - Matini juu ya Zakat. | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza maana na umuhimu wa zakat?<br>(ii) Kubainisha lengo la zakat na namna linavyofikiwa?<br>(iii)Kubainisha sababu kwanini lengo la zakat halifikiwi katika jamii yetu? | 4 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 4.3 Swaumu ya Ramadhani | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza umuhimu wa swaumu.<br>(b) Kubainisha lengo la swaumu.<br>(c) Kufafanua namna swaumu inavyomfanya mwenye kufunga afikie lengo la swaumu.<br>(d) Kubainisha faida za swaumu.<br>(e) Kubainisha sababu kwanini wengi wanaofunga hawafikii lengo la swaumu. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kueleza umuhimu wa swaumu<br>(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya bungua bongo kubainisha lengo la swaumu<br>(iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano Kufafanua namna swaumu inavyomfanya mwenye swaumu.<br>(iv) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kubainisha faida za swaumu<br>(v) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kubainisha sababu kwanini wengi wanaofunga hawafikii lengo la swaumu | - Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza umuhimu wa swaumu?<br>(ii) Kubainisha lengo la swaumu?<br>(iii) Kufafanua namna swaumu inavyomfa nya mwenye kufunga afikie lengo la swaumu?<br>(iv) Kubainisha faida ya swaumu?<br>(v) Kubainisha sababu kwanini wengi wanaofunga hawafikii lengo la swaumu? | 4 |
| | 4.4 Hija | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza umuhimu wa hija.<br>(b) Kubainisha lengo la hija.<br>(c) Kufafanua mafunzo yatokanyo na matendo ya hija.<br>(d) Kueleza sababu kwanini baadhi ya wanaohiji hawafikii lengo la hija. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kueleza umuhimu wa hija.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya bungua bongo kubainisha lengo la hija.<br>(iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kufafanua mafunzo yatokanyo na matendo ya hija.<br>(iv) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kueleza sababu kwanini baadhi ya wanaohiji hawafikii lengo la hija. | -Picha zinazoonesha matendo ya Hijja. | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza umuhimu wa hija?<br>(ii) Kubainisha lengo la hija?<br>(iii) Kufafanua mafunzo yatokanyo na matendo ya hija?<br>(iv) Kueleza sababu kwanini baadhi ya wanaohiji hawafikii lengo la hija? | 4 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 5.0 HAKI NA UADILIFU KATIKA UISLAMU | 5.1 Dhana ya haki na uadilifu katika Uislamu | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza maana ya haki kwa mtazamo wa Uislamu.<br>(b) Kutofautisha kati ya haki na uadilifu.<br>(c) Kutaja misingi ya haki na uadilifu katika Uislamu.<br>(d) Kueleza aina mbalimbali za haki . | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya bungua bongo kueleza maana ya haki kwa mtazamo wa Uislamu.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kutofautisha kati ya haki na uadilifu.<br>(iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kutaja misingi ya haki na uadilifu katika Uislamu<br>(iv) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia njia ya fikiri jadili katika jozi kueleza aina mbalimbali za haki | - Matini za Qura'n<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza maana ya haki kwa mtazamo wa Uislamu?<br>(ii)Kutofautisha kati ya haki na uadilifu?<br>(iii) Kutaja misingi ya haki na uadilifu katika Uislamu?<br>(iv) Kubainisha aina mbalimbali za haki? | 6 |
| | 5.2 Msimamo wa Uislamu juu ya Utumwa. | Mwanafunzi aweze:<br>(a)Kubainisha hali ya utumwa kabla ya Mtume Muhammad(s.a.w).<br>(b)Kueleza jinsi Uislamu ulivyokomesha utumwa wakati na baada ya Mutme Muhammad(s.a.w).<br>(c)Kufafanua upotoshaji wa mahusiano ya utumwa na Uislamu. | (i) Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi wabainishe hali ya utumwa kabla ya Mutme Muhammad s.a.w).<br>(ii)Mwalimu atumie mbinu ya majadiliano kuwaongoza wanafunzi kueleza jinsi Uislamu ulivyokomesha utumwa wakati na baada ya Mtume muhammad(s.a.w).<br>(iii) Kwa kutumia mbinu ya changanya kete mwalimu awaongoze wanafunzi wafafanue upotoshaji wa uhusiano wa utumwa na Uislamu. | -Kielelezo chenye majina ya watumwa walokombolewa na Uislamu. | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kubainisha hali ya utumwa kabla ya Mutme Muhammad(s.a.w)?<br>(ii) Kueleza jinsi Uislamu ulivyokomesha utumwa wakati na baada ya Mtume Muhammad(s.a.w)?<br>(iii)Kufafanua upotoshaji wa mahusiano ya utumwa na Uislamu? | 2 |
| 6.0 QUR'AN | 6.1 Sura za Makkah na Madinah | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kuainisha sura za Makkah na Madinah.<br>(b) Kutofautisha sura za Makkah na madinah | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wafanye mazoezi ya kuanisha sura za Makkah na za Madinah.<br>(ii) Wanafunzi wajadili tofauti kati ya sura za Makkah na Madinah | - Qur'an tukufu<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kuainisha sura za Makkah na Madinah?<br>(ii)Kutofautisha sura za Makkah na Madinah? | 1 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 6.2 Kukusanywa Qur'an katika msahafu | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kuonesha kuwa Qur'an iliwekwa katika msahafu wakati Mtume (s.a.w) na si vinginevyo<br>(b) Kuonesha umuhimu kunakiliwa upya Qur'an wakati wa Uthman(r.a) | (i) Mwalimu awaongze wanafunzi katika vikundi wajadili udhaifu wa hoja za ukusanyaji wa Qur'an wakati wa Abubakar(r.a).<br>(ii)Wanafunzi wajadili umuhimuwa kunakili Qur'an wakati wa Uthman(r.a). | - Qur'an tukufu<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kujadili udhaifu wa hoja za kukusanywa Qur'an wakati wa Abubakar(r.a)?<br>(ii) Kuonesha umuhimu wa kunakiliwa Qur'an wakati wa Uthman(r.a). | 2 |
| | 6.3 Ithibati ya Qur'an kuwa ni kitabu cha Mwenyezi Mungu | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kubainisha hoja za makafiri dhidi ya Qur'an wakati wa Mtume(s.a.w)<br>(b)Kueleza udhaifu wa hoja za makafiri dhidi ya Qur'an wakati wa Mtume(s.a.w). | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wajadili hoja za makafiri dhidi ya Qur'an wakati wa Mtume (s.a.w).<br>(ii) Wanafunzi wajadili udhaifu wa makafiri dhidi ya Qur'an wakati wa Mtume (s.a.w). | msahafu -<br>Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza hoja za makafiri dhidi ya Qur'an wakati wa Mtume(s.a.w)?<br>(ii)Kubainisha udhaifu wa hoja za makafiri dhidi ya Qur'an wakati wa Mtume (s.a.w)? | 4 |
| | 6.4 Sura zilizoteuliwa: Fyl, Humazah, Asr, Takaathur na Bayyinah | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kusoma, kuhifadhi na kutafsiri sura zilizoteuliwa.<br>(b) Kueleza mafunzo yatokanayo na sura zilizoteuliwa. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome sura zilizoteuliwa kwa kuzingatia hukumu<br>(ii) Kwa njia ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi wabaini mafunzo yatokanayo na sura hizo | Msahafu | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kusoma, kuhifadhi na kutafsiri sura zilizoteuliwa?<br>(ii)Kueleza mafunzo yatokanayo na sura zilizoteuliwa? | 6 |

* Makafiri ni *watu wanaopinga kuwepo kwa Mwenyezi Mungu.*

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 7.0 SUNNAH NA HADITH | 7.1 Kukubalika kwa Hadith | (a) Kubainisha hoja juu ya kukubalika kwa Hadith.<br>(b) Kueleza udhaifu wa hoja za wanaopinga Hadith. | (i) Kwa njia ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi wabaini hoja juu ya kukubalika Hadith<br>(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi wajadili katika vikundi udhaifu wa hoja za wanaopinga Hadith. | - Matini juu ya hadith | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kubainisha hoja juu ya kukubalika Hadith?<br>(ii) Kueleza udhaifu wa hoja za wanaopinga Hadith? | 2 |
| | 7.2 Hadith zilizoteuliwa | (a) Kusoma, kuandika na kutafsiri Hadith zilizoteuliwa.<br>(b) Kuchambua mafunzo yatokanyo na Hadith zilizo teuliwa. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome na kutafsiri Hadith zilizoteuliwa.<br>(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi wajadili katika vikundi kuchambua mafunzo yatokanyo na Hadith zilizo teuliwa. | | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kusoma, kuandika na kutafsiri Hadith zilizoteuliwa?.<br>(ii) Kuchambua mafunzo yatokanyo na Hadith zilizo teuliwa? | 4 |
| 8.0 DOLA YA KIISLAMU MADINAH | 8.1 Uanzishwaji wa Dola ya Kiislamu Madinah | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kubainisha hatua alizochukua Mtume (s.a.w) katika kuanzisha Dola ya Kiislamu Madinah.<br>(b) Kuchambua mafunzo yatokanayo na uanzishwaji wa Dola ya Kiislamu Madinah | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wajadili hatua alizochukua Mtume (s.a.w) katika kuanzisha Dola ya Kiislamu, Madinah:<br>- Msikiti kama ofisi<br>- Sekretarieti na shura<br>- Katiba ya Madinah<br>- Mikataba na makabila yaliyozunguka Madinah.<br>- Kuimarisha uchumi na ulinzi.<br>(ii) Kwa njia ya mjadala wa vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi wachambue mafunzo yatokanayo na uanzishwaji wa Dola ya Kiislamu Madinah. | - Matini za historia ya Uislamu.<br>- Bango kitita. | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kubainisha hatua alizochukua Mtume(s.a.w) katika kuanzisha Dola ya Kiislamu-Madinah?<br>(ii)Kuchambua mafunzo yatokanayo na uanzishwaji wa Dola ya Kiislamu Madinah? | 4 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 8.2 Uendeshaji wa Dola ya Kiislamu Madinah. | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza mfumo wa kisiasa na kiuchumi wa Serikali ya Kiislamu Madinah.<br>(b) Kubainisha mfumo wa ulinzi na usalama wa dola ya Kiislamu Madinah.<br>(c) Kujadili mfumo wa diplomasia wa dola ya Kiislamu Madinah. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wajadili katika vikundi mfumo wa kisiasa na kiuchumi wa Serikali ya Kiislamu Madinah<br>(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia fikiri na jadili katika jozi wajadili mfumo wa ulinzi na usalama wa dola ya Kiislamu Madinah<br>(iii) Katika vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kujadili mfumo wa diplomasia wa dola ya Kiislamu Madinah | - Kielelezo kinachoo nesha mfumo wa uendeshaji wa Dola ya Kiislamu Madinah. | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza mfumo wa kisiasa na kiuchumi wa Serikali ya Kiislamu Madinah?<br>(ii) Kubainisha mfumo wa ulinzi na usalama wa dola ya Kiislamu Madinah?<br>(iii) Kujadili mfumo wa diplomasia wa dola ya Kiislamu Madinah? | 4 |
| | 8.3 Upinzani dhidi ya Dola ya Kiislamu. | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kubainisha maadui dhidi ya dola ya Kiislamu Madinah.<br>(b) Kueleza sababu za kutokea vita vya Jihad: (Badr, Uhud, Ahzab, Hunain Muttah na Khaibar).<br>(c) Kufafanua mazingira na matokeo ya vita vya jihad.<br>(d) Kueleza mafunzo yatokanayo na vita vya Jihad: (Badr, Uhud, Ahzab, Hunain Muttah na Khaibar). | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wabainishe maadui wa dola ya Kiislamu.<br>(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi wajadili jinsi sababu zilizopelekea kutokea vita vya Jihad: (Badr, Uhud, Ahzab, Hunain).<br>(iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi wajadili mazingira na matokeo ya vita vya jihad.<br>(iv) Mwalimu awaongoze wanafunzi kujadili mafunzo yatokanayo na vita vya Jihad: (Badr, Uhud, Ahzab, Hunain). | - Matini juu ya Dola ya Kiislamu<br>- Bango kitita<br>- Ramani inayoonesha maeneo vilimopiganwa vita vya Jihad. | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kubainisha maadui dhidi ya dola ya Kiislamu Madinah?<br>(ii) Kueleza sababu zilizosababisha kutokea vita vya Jihad:Badr, Uhud, Ahzab, Hunain, Muttah na Khaibar)?<br>(iii) Kufafanua mazingira na matokeo ya vita vya jihad?<br>(iv) Kueleza mafunzo yatokanayo na vita vya Jihad:(Badr, Uhud, Ahzab, Hunain,Muttah na Khaibar).? | 8 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 8.4 Ushindi wa Waislamu (Fat-hu-Makkah) | Mwanafunzi aweze:<br>(a)Kueleza mazingira yaliyosababisha makubaliano ya mkataba wa Hudaybiyah.<br>(b)Kubainisha vifungu vya mkataba wa Hudaybiyah.<br>(c)Kueleza namna mkataba wa Hudaybiyah ulivyoleta ushindi.<br>(d)Kuchambua mafunzo yatokanayo na mkataba wa Hudaybiyah. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wajadili mazingira yaliyosababisha makubaliano y mkataba wa Hudaybiyah.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome n wabainshe vifungu vya mkataba wa Hudaybiyah.<br>(iii)Wanafunzi wajadili namna Mtume(s.a.w) alivyoikomboa Makkah.<br>(iv) Wanafunzi wabainishemafunzo yatokanayo na mkataba wa Hudaybiyah. | - Matini juu ya Dola ya Kiislamu<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza mazingira yaliyosababisha makubaliano ya mkataba wa Hudaybiyah?<br>(ii)Kueleza kubainisha vifungu vya mkataba wa Hudaybiyah?<br>(iii) Kueleza namna mkataba wa Hudaybiyah ulivyoleta ushindi?<br>(iv) Kuchambua kueleza mafunzo yatokanayo na mkataba wa Hudaybiyah? | 6 |
| | 8.5 Kutawafu kwa Mtume(s.a.w). | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza mafunzo yatokanayo na hija ya kuaga.<br>(b) Kueleza juu ya uzushi wa utume wakati wa Mtume(s.a.w).<br>(c) Kueleza namna waislamu walivyopokea habari za kutawafu Mtume(s.a.w). | Mwalimu awaongoze wanafunzi katika makundi kwa kutumia Hadith na Qur'an wajadili:<br>(i) Mafunzo yatokanayo na Hija ya kuaga.<br>(ii) Uzushi wa Utume wakati wa Mtume(s.a.w).<br>(iii) Hatua walizozichukua waislamu baada ya Mtume(s.a.w) kutawafu. | - Matini za tafsir ya Qur'an<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza mafunzo yatokanayo na hija ya kuaga?<br>(ii)Kueleza juu ya uzushi wa utume wakati wa Mtume (s.a.w)?<br>(iii) Kueleza namna Waislamu walivyopokea habari za kutawafu Mtume (s.a.w)? | 4 |

KIDATO CHA NNE

Ujuzi wa somo la Elimu ya Kiislamu Kidato cha Nne

Baaada ya kumaliza kidato cha  nne mwanafunzi anatarajiwa kuwa na ujuzi wa:

1. Kufafanua nguzo  za nne,tano na sita za imani ya Kiislamu.
2. Kutambua tofauti baina ya Uislamu na dini nyingine.
3. Kuthibitisha mtazamo wa Uislamu juu ya madhehebu.
4. Kufafanua kanuni na taratibu za familia ya Kiislamu.
5. Kupanganua fat-wa ya Uislamu juu ya kudhibiti uzazi.
6. Kugawa mirathi kwa kuzingatia sheria ya Kiislamu.
7. Kubainisha misingi ya sheria,uchumi na siasa katika Uislamu.
8. Kutambua udhaifu wa madai ya makafiri wa leo dhidi ya  Qur'an.
9. Kuchambua mafunzo ya sura zilizoteuliwa.
10. Kutumia mafunzo ya Hadith zilizoteuliwa.
11. Kupambanua mafunzo yatokanayo na historia ya Uislamu baada ya kutawafu Mtume (s.a.w) hadi hivi leo.

Malengo ya Somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu kidato cha nne

Baada ya kumaliza kidato cha Pili mwanafunzi aweze:

1. Kuelewa  nguzo  ya nne,tano na sita za imani ya Kiislamu.
2. Kubainisha tofauti za msingi baina ya Uislamu na Dini nyingine.
3. Kuelewa mtazamo wa Uislamu juu ya madhehebu.
4. Kufafanua kanuni na taratibu za familia ya Kiislamu.
5. Kubaini fat-wa ya Uislamu juu ya kudhibiti uzazi.
6. Kukokotoa mahesabu ya  mirathi kwa kuzingatia sheria ya Kiislamu.
7. Kuelewa  misingi ya sheria,uchumi na siasa katika Uislamu.
8. Kuchambua  udhaifu wa madai ya makafiri wa leo dhidi ya Qur'an.
9. Kuchambua mafunzo ya sura zilizoteuliwa.
10. Kubainisha mafunzo ya Hadith zilizoteuliwa.
11. Kuelewa mafunzo yatokanayo na historia ya Uislamu baada kutawafu Mtume (s.a.w) hadi hivi leo.

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 NGUZO ZA IMANI | 1.1 Kuamini mitume wa Mwenyezi Mungu | Mwanafunzi aweze:<br>(a)Kubaini ushahidi wa kuwepo mitume<br>(b)Kueleza umuhimu wa kuamini mitume wa Mwenyezi Mungu.<br>(c)Kufafanua sifa na lengo la kuletwa mitume.<br>(d)Kueleza sababu kwanini hapana mtume baada ya Muhammad (s.a.w).<br>(e)Kueleza maana halisi ya kuamini mitume wa Mwenyezi Mungu katika maisha ya kila siku. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kueleza umuhimu wa kuamini mitume wa Mwenyezi Mungu.<br>(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kufafanua sifa na kazi za mitume.<br>(iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kueleza sababu kwanini hapana mtume baada ya Muhammad(s.a.w).<br>(iv) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kueleza maana halisi ya kuamini mitume katika maisha ya kila siku. | Matini za Qur'an juu ya Imani<br><br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza :<br>(i) Kubaini ushahidi wa kuwepo mitume?<br>(ii) Kueleza umuhimu wa kuamini mitume wa Mwenyezi Mungu?<br>(iii) Kufafanua sifa na lengo la kuletwa mitume?<br>(iv) Kueleza sababu kwanini hapana mtume baada ya Muhammad (s.a.w)?<br>(v) Kueleza maana halisi ya kuamini mitume wa Mwenyezi Mungu katika maisha ya kila siku? | 4 |
| | 1.2 Kuamini siku ya mwisho | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kufafanua mazingira ya siku ya mwisho<br>(b) Kubainisha madai ya makafiri dhidi ya kuwepo siku ya malipo na udhaifu wa madai hayo.<br>(c) Kueleza hoja za kuthibitisha kuwepo siku ya malipo.<br>(d) Kueleza maana halisi ya kuamini siku ya malipo.<br>(e) Kueleza dhana ya shufaa siku ya malipo | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kufafanua mazingira ya siku ya mwisho<br>(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kubainisha madai ya makafiri dhidi ya kuwepo siku ya malipo na udhaifu wa madai hayo.<br>(iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kueleza hoja za kuwepo siku ya malipo.<br>(iv) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya bungua bongo kueleza maana halisi ya kuamini siku ya malipo. | Matini za Qur'an juu ya Imani<br><br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kufafanua mazingira ya siku ya mwisho?<br>(ii) Kubainisha madai ya makafiri dhidi ya kuwepo siku ya malipo na udhaifu wa madai hayo?<br>(iii) Kueleza hoja za kuthibitisha kuwepo siku ya malipo?<br>(iv) Kueleza maana halisi ya kuamini siku ya malipo?<br>(v) Kueleza dhana ya shufaa siku ya malipo? | 4 |

* Makafiri ni *watu wanaopinga kuwepo kwa Mwenyezi Mungu.*

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1.3 Kuamini Qadar ya Mwenyezi Mungu. | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza maana ya Qadar na Qudra ya Mwenyezi Mungu.<br>(b) Kubainisha umuhimu wa kuamini Qadar.<br>(c) Kueleza mtazamo wa Uislamu juu ya Qadar.<br>(d) Kueleza maana halisi ya kuamini Qadar ya Mwenyezi Mungu katika maisha ya kila siku. | (i) Kwa mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi waeleze maana ya Qadar na Qudra ya Mwenyezi Mungu.<br>(ii)Kwa mbinu ya bungua bongo mwalimu awaongoze wanafunzi wabainishe umuhimu wa kuamini Qadar ya Mwenyezi Mungu. | - Matini ya Qadar ya Mwenyezi Mungu. | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza maana ya Qadar na Qudra na Mwenyezi Mungu?<br>(ii) Kubainisha umuhimu wa kuamini Qadar?<br>(iii) Kueleza mtazamo wa Uislamu juu ya Qadar?<br>(iv) Kueleza maana halisi ya kuamini Qadar ya Mwenyezi Mungu katika maisha ya kila siku? | 4 |
| 2.0 MTAZAMO WA UISLAMU JUU YA DINI | 2.1 Makundi makuu ya Dini yaliyotajwa katika Qur'an. | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kubainisha makundi makuu ya Dini.<br>(b) Kueleza tofauti zilizopo kati ya Uislamu na Dini nyingine (Ukafiri, Ushirikina na Utawa).<br>(c) Kuchanganua madhara ya ukafiri, ushirikina na utawa. | (i) Kwa mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi wabainishe makundi makuu ya Dini.<br>(ii)Kwa mbinu ya bugua bongo mwalimu awaongoze wanafunzi waeleze tofauti zilizopo kati ya Uislamu na Dini nyingine.<br>(iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi wachanganue madhara ya ukafiri, ushirikina na utawa. | -Matini za makundi makuu ya Dini. | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kubainisha makundi makuu ya Dini?<br>(ii)Kueleza tofauti zilizopo kati ya Uislamu na Dini nyingine (Ukafiri, Ushirikina na Utawa)?<br>(iii) Kuchanganua madhara ya ukafiri, ushirikina na utawa? | 2 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3.0 CHIMBUKO LA FIQH | 3.1 Mgawanyiko wa madhehebu | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kubainisha sababu zilizopelekea kutokea madhehebu<br>(b) Kueleza msimamo wa Uislamu juu ya madhehebu. | (i) Wanafunzi wakiongozwa na mwalimu wajadili sababu zilizopelekea kutokea madhehebu<br>(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kwa kurejea Qur'an na Hadith kueleza msimamo wa Uislamu juu ya madhehebu | - Kielelezo cha kuonesha majina ya madhehebu mbali mbali. | (i) Kubainisha sababu zilizopelekea kutokea madhehebu?<br>(ii) Kueleza msimamo wa Uislamu juu ya madhehebu? | 2 |
| 4.0 FAMILIA YA KIISLAMU | 4.1 Ndoa katika Uislamu | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza maana ya ndoa katika Uislamu.<br>(b) Kubainisha taratibu za kuoa Kiislamu.<br>(c) Kubainisha majukumu katika familia.<br>(d) Kueleza mtazamo wa Qur'an juu ya kuoa mke zaidi ya mmoja. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya bungua bongo kueleza maana ya ndoa katika Uislamu.<br>(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia fikiri na jadili katika jozi kubainisha taratibu za kuoa kiislamu.<br>(iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kubainisha majukumu katika familia.<br>(iv) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kueleza mtazamo wa Qur'an juu ya kuoa mke zaidi ya mmoja | - Matini juu ya Familia ya Kiislamu<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza maana na ya ndoa katika Uislamu?<br>(ii) Kubainisha taratibu za kuoa Kiislamu?<br>(iii) Kubainisha majukumu katika familia kueleza mtazamo wa Qur'an juu ya kuoa mke zaidi ya mmoja?<br>(iv) Kueleza mtazamo wa Qur'an juu ya kuoa mke zaidi ya mmoja? | 6 |
| | 4.2 Kudhibiti uzazi katika Uislamu | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza nadharia juu ya kampeni ya kikafiri ya kudhibiti uzazi na madhara yake.<br>(b) Kubainisha mtazamo wa Uislamu juu ya kudhibiti uzazi. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kueleza nadharia juu ya kudhibiti uzazi na madhara yake.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia fikiri na jadili katika jozi kubainisha mtazamo wa uislamu juu ya kudhibiti uzazi.<br>- | - Matini juu ya Familia ya Kiislamu<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza nadharia juu ya kampeni ya kikafiri ya kudhibiti uzazi na madhara yake?<br>(ii)Kubainisha mtazamo wa Uislamu juu ya kudhibiti uzazi? | 4 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 4.3 Talaka na Eda | Mwanafunzi aweze :<br>(a) Kueleza dhana ya talaka na hekima yake.<br>(b) Kueleza taratibu za suluhu kati ya mke na mume.<br>(c) Kufafanua aina za talaka<br>(d) kueleza taratibu za talaka.<br>(e) Kutofautisha kati ya eda ya kuachwa na eda ya kufiwa. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia ya bungua bongo kueleza dhana ya talaka na hekima yake.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kueleza taratibu za suluhu kati ya mke na mume.<br>(iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia maswali na majibu kufafanua aina za talaka.<br>(iv) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kueleza taratibu za talaka.<br>(v) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano kutofautisha kati ya eda ya kuachwa na eda ya kufiwa. | - Matini juu ya familia ya Kiislamu<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza dhana ya talaka na hekima yake?<br>(ii)Kueleza taratibu za suluhu kati ya mke na mume?<br>(iii) Kufafanua aina za talaka?<br>(iv) Kueleza taratibu za talaka?<br>(v) Kutofautisha kati ya eda ya kuachwa na eda ya kufiwa? | 4 |
| | 4.4 Mirathi katika Uislamu | Mwanafunzi aweze :<br>(a) Kueleza maana ya mirathi na umuhimu wa kugawa mirathi Kiislamu.<br>(b) kukokotoa hesabu za mirathi.<br>(c) Kueleza hekima ya sheria ya Mirathi ya Kiislamu.<br>(d) Kueleza kwa ufupi udhaifu wa sheria ya kitwaghuti ya mirath | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya bungua bongo kueleza maana ya mirathi na umuhimu wa kugawa mirathi Kiislamu.<br>(ii)Wanafunzi wafanye Hesabu mbalimbali kuhsu mirathi.<br>(iii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi wajadili hekima ya sheria ya Mirathi ya Kiislamu.<br>(iv) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kueleza kwa ufupi udhaifu wa sheria ya kitwaghuti ya mirath. | - Matini juu ya Familia ya Kiislamu<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza maana ya mirathi na umuhimu wa kugawa mirathi Kiislamu?<br>(ii)Kukokotoa mahesabu ya mirathi?<br>(iii) Kueleza hekima ya sheria ya Mirathi ya kiislamu?<br>(iv) Kueleza kwa ufupi udhaifu wa sheria ya kitwaghuti ya mirathi? | 6 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 4.5 Hadhi na Haki za mwanamke katika Uislamu | Mwanafunzi aweze :<br>(a) Kueleza hadhi na haki za mwanamke katika jamii za kijahili.<br>(b) Kueleza hifadhi ya mwanamke katika Uislamu na hekima yake<br>( c) Kubainisha haki za mwanamke zitolewazo na Uislamu | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi wajadili hadhi na haki za mwanamke katika jamii ya kijahili.<br>(ii) Wanafunzi wajadili hifadhi ya mwanamke katika Uislamu na hekima yake<br>(iii) Kwa maswali na majibu wanafunzi wabainishe haki za mwanamke zitolewazo na Uislamu | - Matini juu ya Familia ya Kiislamu<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza hadhi na haki za mwanamke katika jamii ya kijahili?<br>(ii) Kueleza hifadhi ya mwanamke katika Uislamu na hekima yake?<br>(iii)Kubainisha haki za mwanamke zitolewazo na Uislamu? | 4 |
| 5.0 MFUMO WA JAMII YA KIISLAMU. | 5.1 Misingi na Maadili katika Uislamu. | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kutofautisha kati ya mtazamo wa Uislamu na mtazamo wa kitwaghuti juu ya maadili.<br>(b) Kutaja misingi ya maadili ya Uislamu | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia bungua bongo kutofautisha kati ya mtazamo wa Uislamu na mtazamo wa kitwaghut juu ya maadili<br>(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia maswali na majibu kutaja misingi ya maadili ya Uislamu | - Matini juu ya Maadili katika Kiislamu<br>- Bango kitita | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kutofautisha kati ya mtazamo wa Uislamu na mtazamo wa kitwaghuti juu ya maadili.<br>(ii)Kutaja misingi ya maadili ya Uislamu. | 3 |
| | 5.2 Sheria katika Uislamu | Mwanafunzi aweze:<br>(a)Kueleza maana ya sheria.<br>(b)Kubainisha kazi ya sheria katika jamii.<br>(c)Kuainisha mgawanyo wa makosa na adhabu zake katika sheira ya Kiislamu.<br>(d)Kueleza tofauti ya chimbuko la sheira za Kiislamu na zile za Kitwaghuti.<br>(e)Kubainisha haki za makundi makundi ya watu mbalimbali katika dola ya Kiislamu. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia bungua bongo kueleza maana ya sheria na kazi ya sheria katika jamii.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi kueleza tofauti ya chimbuko la sheria za Kiislamu na zile za kitwaghuti.<br>(iii) Mwanafunzi wajadili<br>- Mgawanyo wa makosa na adhabu zake katika sheria ya Kiislamu.<br>- Haki za makundi ya watu mbalimbali katika dola ya kiislamu | - Mtini juu ya Maadili katika Uislamu.<br>- Bango kitita. | Je mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kueleza maana ya sheria?<br>(ii) Kubainisha kazi ya sheria katika jamii?<br>(iii)Kuainisha mgawanyo wa makosa na adhabu zake katika sheira ya Kiislamu?<br>(iv)Kueleza tofauti ya chimbuko la sheira za Kiislamu na zile za Kitwaghuti?<br>(v)Kubainisha haki za makundi ya watu mbalimbali katika dola ya Kiislamu? | 6 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 5.3 Uchumi katika Uislamu. | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kutofautisha kati ya mfumo wa uchumi wa Kiislamu na ule wa kikafiri.<br>(b) Kubainisha njia za halali za uchumi na za haramu.<br>(c) Kubainisha uharamu wa riba na madhara yake.<br>(d) Kueleza namna ya kuendesha taasisi za fedha kwa kufuata sheria za Kiislamu. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi kutofautisha kati ya mfumo wa uchumi wa Kiislamu na ule wa Kikafiri.<br>(ii)Mwanafunzi wajadili njia za halali za uchumi.<br>(iii) Mwalimu awaongoze wananfunzi kwa kutumia fikiri-jadili katika jozi kujadili madhara ya riba.<br>(iv) Mwalimu amwalike mtaalamu kuja kuzungumza na wanafunzi juu ya uendeshaji Taasisi za fedha Kiislamu. | -Matini juu ya Uchumi katika Uislamu.<br>-Bango kitita. | Je,wanafunzi wameweza:<br>(i) Kutofautisha kati ya mfumo wa uchumi wa Kiislamu na ule wa kikafiri.<br>(ii)Kubainisha njia za halali za uchumi na za haramu.<br>(iii) Kubainisha uharamu wa riba na madhara yake.<br>Kueleza namna ya kuendesha taasisi za fedha kwa kufuata sheria za Kiislamu. | 4 |
| | 5.4 Siasa na Uendeshaji wa Dola. | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kueleza maana ya siasa na Dola kwa mtazamo wa kikafiri.<br>(b) Kubainisha msonge wa uongozi katika Uislamu.<br>(c) Kuchambua sifa za kiongozi katika Uislamu.<br>(d) Kueleza haki mbalimbali za raia katika Dola ya Kiislamu. | (i) Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi waeleze maana ya siasa na maana ya Dola kwa mtazamo wa kikafiri na ule wa Kiislamu.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi wabainishe msonge wa uongozi katika Uislamu.<br>(iii)Kwa kutumia mbinu ya fikirisha jozisha mwalimu awaongoze wanafunzi wachambue sifa za kiongozi katika Uislamu.<br>(iv) Mwalimu aongoze majadiliano wanafunzi waeleze haki mbalimbali za raia katika Dola ya Kiislamu. | - Kielelezo kinachoone sha msonge wa uongozi katika Uislamu. | Je, wanafunzi wameweza:<br>(i) Kueleza maana ya siasa na Dola kwa mtazamo wa kikafiri?<br>(ii)Kubainisha msonge wa uongozi katika Uislamu?<br>(iii) Kuchambua sifa za kiongozi katika Uislamu?<br>(iv) Kueleza haki mbalimbali za raia katika Dola ya Kiislamu? | 4 |

* Makafiri ni *watu wanaopinga kuwepo kwa Mwenyezi Mungu.*

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 6.0 QUR'AN | 6.1 Ithibati ya Qur'an | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kubainisha madai ya makafiri dhidi ya Qur'an.<br>(b) Kueleza udhaifu wa madai ya makafiri wa leo dhidi ya Qur'an.<br>(c) Kufafanua hoja zinazothibitisha kuwa Qur'an ni neno la Allah (s.w). | (i) Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi wabainishe madai ya makafiri dhidi ya Qur'an.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi wajadili udhaifu wa madai ya Makafiri dhidi ya Qur'an.<br>(iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi wafafanue hoja kuwa Qur'an ni neno la Allah(s.w). | - Msahafu wa Tafsiri.<br>- Kitabu cha kiada cha kidato cha IV. | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kubainisha madai ya makafiri dhidi ya Qur'an?<br>(ii)Kueleza udhaifu wa madai ya makafiri wa leo dhidi ya Qur'an?<br>(iii) Kufafanua hoja zinazothibitisha kuwa Qur'an ni neno la Allah(s.w)? | 4 |
| | 6.2 Sura zilizoteuliwa:<br>- Tyn<br>- Nashrah<br>- Dhuha<br>- A'alaa | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kusoma na kuhifadhi sura zilizoteuliwa.<br>(b) Kutafsiri sura zilizoteuliwa.<br>(c) Kuchambua mafunzo yatokanayo na sura zilizoteuliwa. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi na kisha mmoja mmoja wasome na kuhifadhi sura zilizoteuliwa.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi wanafunzi watafsiri sura zilizoteuliwa.<br>(iii) Kwa kutumia njia ya fikiri-jadili katika jozi mwalimu awaongoze wanafunzi wachambue mafunzo yatokanayo na sura zilizoteuliwa. | - Msahafu wa tafsiri. | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kusoma na kuhifadhi sura zilizoteuliwa?<br>(ii)Kutafsiri sura zilizoteuliwa?<br>(iii) Kuchambua mafunzo yatokanayo na sura zilizoteuliwa? | 6 |
| 7.0 SUNNAH NA HADITH | 7.1 Hadith zilizoteuliwa. | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kusoma na kuhifadhi Hadith zilizoteuliwa.<br>(b) Kutafsiri na kuandika Hadith zilizoteuliwa.<br>(c) Kuchambua mafunzo ya Hadith zilizoteuliwa. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi wasome na kuhifadhi Hadith zilizoteuliwa.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi watafsiri Hadith zilizoteuliwa kisha waziandike kwenye madaftari.<br>(iii) Kwa kutumia mbinu ya fikiri-jadili kaitka jozi mwalimu awaongoze wanafunzi wachambue mafunzo ya Hadith zilizoteuliwa kisha wayaandike katika daftari zao. | - Vitabu mbalimbali vya Hadith za Mtume Muhammad (s.a.w). | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kusoma na kuhifadhi Hadith zilizoteuliwa?<br>(ii)Kutafsiri na kuandika Hadith zilizoteuliwa?<br>(iii) Kuchambua mafunzo ya Hadith zilizoteuliwa? | 4 |

* Makafiri ni *watu wanaopinga kuwepo kwa Mwenyezi Mungu.*

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 8.0 HISTORIA YA UISLAMU BAADA YA KUTAWAFU MTUME (S.A.W) HADI HIVI LEO. | 8.1 Ukuaji na Uendeshaji wa Dola ya kiislamu wakati wa Makhalifa wanne waongofu. | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kubainisha makhalifa wanne waongofu.<br>(b) Kuainisha taratibu zilizotumika kuwapata makhalifa waongofu.<br>(c) Kueleza sababu zilizopelekea kupanuka kwa dola ya Kiislamu.<br>(d) Kubainisha sababu zilizopelekea Riddah.<br>(e) Kueleza mfumo wa uongozi, uchumi, ulinzi, na mahusiano ya kimataifa.<br>(f) Kuchanganua sababu zilizopelekea kuporomoka kwa Dola ya Kiislamu na mafunzo yatokanayo. | (i) Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo mwalimu awaongoze wanafunzi wabainishe makhalifa wanne waongofu.<br>(ii)Kwa njia ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi waainishe taratibu zilizotumika kuwapata makhalifa waongofu.<br>(iii) Kwa njia ya fikiri-jadili katika jozi mwalimu awaongoze wanafunzi waeleze sababu zilizopelekea kupanuka kwa dola ya Kiislamu.<br>(iv) Mwalimu awaongoze wanafunzi mmoja mmoja wabainishe sababu zilizopelekea Riddah.<br>(v) Mwlaimu awaongoze wanafunzi katika vikundi waeleze mfumo wa uongozi, uchumi, ulinzi na mahusiano ya Kimataifa.<br>(vi) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi wavhangamue sababu zilizopelekea kuporomoka kwa Dola ya Kiislamu na mafunzo yatokanayo. | -Matini za Historia ya Uislamu wakati wa Makhalifa. | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kubainisha makhalifa wanne waongofu?<br>(ii)Kuainisha taratibu zilizotumika kuwapata makhalifa waongofu?<br>(iii)Kueleza sababu zilizopelekea kupanuka kwa dola ya Kiislamu?<br>(iv) Kubainisha sababu zilizopelekea Riddah?<br>(v)Kueleza mfumo wa uongozo, uchumi, ulinzi, na mahusiano ya Kimataifa?<br>(vi)Kuchanganua sababu zilizopelekea kuporomoka kwa Dola ya Kiislamu na mafunzo yatokanayo? | 8 |
| | 8.2 Uanzishwaji wa makundi ya harakati za kuhuisha uislamu ulimwenguni. | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kubainisha makundi mbalimbali maarufu ya harakati za kuhuisha Uislamu.<br>(b) Kuchambua mbinu zilizotumiwa na makundi ya harakati za kuhuisha Uislamu.<br>(c) Kueleza mafunzo yatokanayo na jitihada za makundi ya kuhuisha Uislamu. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa mbinu ya maswali na majibu wabainishe makundi mbalimbali ya harakati za kuhuisha Uislamu.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi wachambue mbinu zilizotumiwa na makundi ya harakati za kuhuisha Uislamu.<br>(iii) Kwa kutumia mbinu ya fikirisha-jozisha mwalimu awaongoze wanafunzi waeleze mafunzo yatokanayo na jitihada za makundi ya kuhuisha Uislamu. | - Matini za Historia ya Uislamu. | Je, mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kubainisha makundi mbalimbali ya harakati za kuhuisha Uislamu?<br>(ii) Kuchambua mbinu zilizotumiwa na makundi ya harakati za kuhuisha Uislamu?<br>(iii)Kueleza mafunzo yatokanayo na jitihada za makundi ya kuhuisha Uislamu? | 6 |

| MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 8.3 Kuingia kwa Uislamu Tanzania na Afrika Mashariki. | Mwanafunzi aweze:<br>(a) Kubainisha namna Uislamu ulivyoingia Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla.<br>(b) Kueleza nguvu ya Uislamu ilivyokuwa kabla, wakati na baada ya ukoloni nchini Tanzania na Afrika Mashariki.<br>(c) Kubainisha nguvu ya upinzani dhidi ya Uislamu Tanzania na Afrika Mashariki.<br>(d) Kueleza jitihada za kuhuisha Uislamu Tanzania na Afrika Mashariki hivi leo. | (i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa mbinu ya maswali na majibu wabainishe namna Uislamu ulivyoingia Tanzania na Afrika Mashariki.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi mmoja mmoja waeleze nguvu za Uislamu wakati na baada ya ukoloni nchini Tanzania na Afrika Mashariki.<br>(i) Kwa kutumia mbinu ya fikiri-jadili katika jozi mwalimu awaongoze wanafunzi wabainishe upinzani dhidi ya Uislamu Tanzania na Afrika Mashariki.<br>(ii)Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi waeleze jitihada za kuhuisha Uislamu Tanzania na Afrika Mashariki. | - Matini za Historia ya Uislamu Afrika Mashariki na Tanzania. | Je mwanafunzi ameweza:<br>(i) Kubainisha namna Uislamu ulivyoingia Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla?<br>(ii) Kueleza nguvu ya Uislamu kabla,wakati na baada ya ukoloni nchini Tanzania na Afrika Mashariki?<br>(iii)Kubainisha nguvu ya upinzani dhidi ya Uislamu Tanzania na Afrika Mashariki?<br>(iv)Kueleza jitihada za kuhuisha Uislamu Tanzania na Afrika Mashariki hivi leo? | 6 |

Wabillah Tawfiiq